JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA


# WIZARA YA AFYA

*Idara ya Kinga · Sehemu ya Epidemiolojia na Udhibiti wa Magonjwa*

**WIKI 35 · 2026**

# JARIDA LA TAARIFA YA MAGONJWA KWA JAMII

**24 — 30 Agosti 2026**




**Ramani ya Tanzania, ikionesha mchanganuo wa magonjwa ya mlipuko na matukio yenye athari kiafya yaliyojitokeza katika mikoa mbalimbali, wiki ya kiepidemiolojia ya 35, 2026.**

| 510 | 4 | 224 | 14 | 6 | 30 |
|---|---|---|---|---|---|
| Matukio ya Kung'atwa na Mbwa/Paka | Visa vya ugonjwa wa Surua | Matukio ya Kung'atwa na Nyoka | Visa vya Homa ya Dengue | Visa vya Uviko-19 na Influenza | Visa vya Kuhara (Rota) |

# 📖 Yaliyomo


1 Magonjwa ya Mlipuko na Matukio yenye Athari za Kiafya Duniani Uk. 2
2 Magonjwa ya Mfumo wa Njia ya Hewa Uk. 3
3 Magonjwa Yanayozuilika kwa Chanjo Uk. 4
4 Kung'atwa na Mnyama Jamii ya Mbwa/Paka Uk. 5
5 Kung'atwa na Nyoka Uk. 6
6 Homa ya Dengue Uk. 7
7 Ugonjwa wa Kuhara wa Virusi vya Rota Uk. 8


## 💬 Kwa Nini Jarida Hili?

Kila wiki, Wizara ya Afya inafuatilia magonjwa yanayoweza kuathiri jamii yetu. Jarida hili linakupa taarifa fupi na sahihi kuhusu magonjwa na matukio haya, hatua ambazo Serikali inachukua na muhimu zaidi unachoweza kufanya wewe kujikinga na kulinda familia yako.

### 🌍 Magonjwa ya Mlipuko na Matukio yenye Athari za Kiafya Duniani

**Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo:** Mlipuko wa ugonjwa wa Ebola aina ya Bundibugyo umekuwa tishio kubwa, visa vikifikia 5,863 vikiwemo vifo 2,824, Mkoa wa Ituri umendelea kuwa kitovu cha mlipuko.
Ugonjwa wa Kipindupindu umeendelea kuenea ambapo visa vinavyoshukiwa vilifikia 39,483 na vifo 1,173, huku upungufu wa maji salama na migogoro ikiathiri juhudi za udhibiti.

**Bangladesh:** Mlipuko wa ugonjwa wa Surua umendelea, ukiwa na zaidi ya visa 18,000 vilivyothibitishwa na vifo 938.

**Kenya:** Ugonjwa wa Homa ya Dengue umeendelea kuongezeka, visa 1,678 vya homa ya Dengue katika kaunti za Garissa na Wajir

**Australia:** Mlipuko wa ugonjwa wa Dondakoo, wenye visa 538, kiwango cha juu zaidi tangu kumbukumbu zilipoanza.

**Ugiriki:** Visa 232 vya virusi vya West Nile, vikiwemo visa vya madhara kwenye mfumo wa fahamu na vifo 19 vimetolewa taarifa.

**Nepal:** Mafuriko makubwa nchini yaliosababisha mamia ya vifo na zaidi ya watu 1,300 kutoweka.

# Magonjwa ya Mfumo wa Njia ya Hewa

Kwa wiki hii, jumla ya sampuli 111 za wagonjwa wa mfumo wa njia ya hewa zilipimwa vipimo vya Influenza na UVIKO-19. Majibu yanaonesha uwepo wa kiwango kidogo cha maambukizi ya Influenza na UVIKO-19 katika miezi ya Januari mpaka Aprili ukilinganisha na miezi mingine, mwenendo ambao umeonekana hata kwa miaka iliyopita.

| 4/111 (3.6%) | 2/111 (1.8%) | 0 |
|---|---|---|
| Sampuli chanya za UVIKO-19 | Sampuli chanya za Influenza | Vifo |

## Wagonjwa Waliothibitika Wanatoka Katika Mikoa ya;

- Dar es Salaam
- Mbeya
- Tabora
- Morogoro

## Dalili za Kuzingatia

- 🤕 Kuumwa Kichwa
- 🌡️ Homa
- 😮 Uchovu
- 😷 Kikohozi
- 🤧 Mafua

## Hatua Zinazoendelea Kuchukuliwa

✔️ Kuimarisha ufuatiliaji katika vituo vya uangalizi kwa kuchukua sampuli za wagonjwa wenye dalili husika.

### 👌 Wito kwa Jamii

→ Nawa mikono mara kwa mara kwa sabuni na maji safi, au tumia vitakasa mikono.

→ Funika mdomo na pua (tumia tishu au kiwiko cha mkono) unapokohoa/kupiga chafya.

→ Fika kituo cha kutolea huduma ya afya mapema endapo una homa, kikohozi, mafua makali au kupumua kwa shida.

# Magonjwa Yanayozuilika kwa Chanjo

Sampuli 4 kati ya 84 (4.8%) zilionesha uwepo wa vimelea vya Surua wiki hii. Idadi hii haijafikia kiwango cha mlipuko, lakini uangalizi unaendelea.

| 4/84 (4.8%) | 0 |
| --- | --- |
| Sampuli chanya za Surua | Vifo |

## Sampuli Chanya ni Kutoka Halmashauri ya;

- Wilaya ya Kakonko — **Kisa 1**
- Wilaya ya Chunya — **Visa 2**
- Wilaya ya Karagwe — **Kisa 1**

## Dalili za Kuzingatia

- **Homa Kali**
- **Macho Mekundu**
- **Mafua/Kikohozi**
-  **Vipele Mwilini**

## Hatua Zilizoendelea Kuchukuliwa

✔️ Utoaji wa chanjo kwa watoto wote walio katika umri wa kupata chanjo.

✔️ Kutoa elimu kwa jamii kuhusu ugonjwa na umuhimu wa chanjo.

✔️ Kutoa matibabu sahihi kwa wagonjwa wote wenye dalili za ugonjwa yanayoweza kuzuilika kwa chanjo.

✔️ Utoaji wa matone ya Vitamin A kwa watoto wanaopatiwa chanjo.

### 👌 Wito kwa Jamii

→ Peleka mtoto wako kwenye chanjo kwa kufuata ratiba yake.

→ Toa taarifa haraka pale mtoto anapoonesha dalili za ugonjwa.

→ Shiriki kikamilifu kwenye kampeni za chanjo zinazofanyika jirani yako.

# Kung'atwa na Mnyama Jamii ya Mbwa/Paka

Matukio ya watu 510 ya kung'atwa na mnyama jamii ya Mbwa au Paka wanaoweza kusababisha ugonjwa wa Kichaa cha Mbwa, bila kifo yametolewa taarifa wiki hii ya 35. Idadi hii imepungua kwa asilimia 4.5 ikilinganishwa na matukio ya watu 534 kung'atwa na mnyama jamii ya Mbwa au Paka yaliyotolewa taarifa wiki ya 34

| 510 | ↓ | 0 |
|---|---|---|
| Watu waliong'atwa na Mbwa/Paka | Imepungua kwa 4.5% ukilinganisha na wiki iliyopita | Vifo |

## Mikoa Yenye Matukio Mengi ya Kung'atwa na Mnyama Jamii ya Mbwa/Paka kwa wiki hii

Pwani — **56** Mwanza — **49** Dodoma — **47** Mara — **34** Lindi — **29**

## Uking'atwa na Mnyama, Fanya Yafuatayo;

**Uking'atwa na Mnyama** → **Osha Jeraha kwa Sabuni na Maji** → **Nenda Kituo cha kutolea huduma za Afya Haraka**

## Hatua Zinazoendelea Kuchukulia

✔️ Kuimarisha upatikanaji wa chanjo ya Kichaa cha Mbwa kwa binadamu.

✔️ Wahudumu wa afya kuendelea kutoa elimu kuhusu kujikinga na hatua za kuchukua baada ya kung'atwa na mnyama jamii ya Mbwa/Paka.

### 👌 Wito kwa Jamii

→ Osha jeraha kwa sabuni na maji mengi kabla ya kwenda kituo cha kutolea huduma ya afya; usifunge jeraha.

→ Fika kituo cha kutolea huduma za afya mara moja kwa ajili ya kupata matibabu na chanjo pale inapohitajika.

→ Wamiliki wa Mbwa/Paka wachanje wanyama chanjo dhidi ya Kichaa cha Mbwa kila mwaka.

# Kung'atwa na Nyoka

Jumla ya watu 224 wametolewa taarifa ya kung'atwa na Nyoka bila kifo katika wiki ya 35. Idadi hii imepungua kwa asilimia 10.4 ikilinganishwa na matukio ya kung'atwa na Nyoka 250 ya wiki ya 34.

| 224 | ↓ | 0 |
|---|---|---|
| Watu waliong'atwa na Nyoka wiki hii | Kupungua kwa 10.4% ukilinganisha na wiki iliyopita | Vifo |

## Mikoa Yenye Matukio Mengi ya Kung'atwa na Nyoka kwa wiki hii

Njombe — **24** | Songwe — **23** | Tanga — **21** | Mwanza — **17** | Morogoro — **14**

## Jikinge Ukiwa Nyumbani

- **Tumia Mwanga Usiku**
- **Safisha Mazingira Yanayokuzunguka**
- **Vaa Mabuti/Glavu**
- **Lala Katika Kitanda Kilicho Juu**

## Hatua Zinazoendelea Kuchukuliwa

✔️ Taarifa hizi zinatumika kuhakikisha upatikanaji wa dawa kinga dhidi ya sumu ya nyoka (anti-venoms).

### 👌 Wito kwa Jamii

→ Nenda kituo cha kutolea huduma za afya mara moja endapo utang'atwa na Nyoka; usipoteze muda.

→ Usitumie dawa za kienyeji wala kubana mshipa wa damu kwenye jeraha.

→ Kumbuka muonekano wa nyoka (rangi/umbo) bila kuhatarisha usalama wako itasaidia matibabu.

# Homa ya Dengue

Kwa wiki ya 35, Wizara imepokea taarifa ya wagonjwa 14 kutoka Mkoa wa Dar es Salaam na mgonjwa mmoja Mkoa wa Pwani idadi hii imeongezeka ukilinganisha na wiki iliyopita ambapo kulikuwa na wagonjwa 9.

| | | |
|---|---|---|
| **14**<br>Wagonjwa wiki hii | ⬆<br>Kuongezeka kwa kiwango cha wagonjwa ukilinganisha na wiki iliyopita (55.6%) | **0**<br>Vifo |

## Mikoa Iliyotoa Taarifa ya Wagonjwa

Dar es Salaam

Pwani

## Dalili za Kuzingatia

- Homa ya Ghafla
- Maumivu ya Viungo
- Uchovu Mkali
- Maumivu ya Kichwa

## Hatua Zinazoendelea Kuchukuliwa

✔️ Kuongeza upatikanaji wa vipimo dhidi ya ugonjwa wa Homa ya Dengue katika vituo vya kutolea huduma za afya.

✔️ Kushirikiana na Halmashauri na wadau kuhakikisha usafi wa mazingira.

### 👌 Wito kwa Jamii

→ Funika maji kwenye madumu, mapipa na vyombo vingine.

→ Weka mazingira safi; ondoa taka zinazoweza kuzalisha Mbu.

→ Fika kituo cha kutolea huduma za afya haraka ukipata homa ya ghafla, maumivu ya viungo, au uchovu usio wa kawaida.

# 🚰 Ugonjwa wa Kuhara wa Virusi vya Rota

Mlipuko wa virusi vya Rota umeripotiwa katika Halmashauri ya Mji wa Mafinga, Mkoa wa Iringa tangu tarehe 14 Agosti 2026, ukifikia jumla ya wagonjwa 89. Kwa wiki hii wagonjwa 30 wametolewa taarifa, ambapo mpaka sasa hamna vifo vilivyotolewa taarifa.

| 30 | 0 |
|---|---|
| Wagonjwa wiki hii (Mji wa Mafinga) | Vifo |

## Wagonjwa Waliothibitika Wanatoka Katika Mkoa wa;

Iringa

## Dalili za Kuzingatia

- 🚽 **Kuhara**
- 🤢 **Kutapika**
- 🌡️ **Homa**

## Hatua Zilizoendelea Kuchukuliwa

✔️ Kuhakikisha upatikanaji wa dawa na vifaa muhimu kwa ajili ya matibabu ya ugonjwa wa kuhara.

✔️ Kufuatilia na kuchanja watoto wasiochanjwa au waliopata chanjo pungufu.

✔️ Kuimarisha ufuatiliaji wa ugonjwa, pamoja na afua za maji na usafi wa mazingira.

### 👌 Wito kwa Jamii

→ Nawa mikono kwa sabuni kabla ya kula na baada ya kutumia choo; wafundishe watoto pia.

→ Tumia maji safi na salama ya kunywa.

→ Fika kituo cha kutolea huduma za afya haraka endapo mtoto anahara, kutapika mfululizo, au dalili za upungufu wa maji mwilini (mfano macho kuingia ndani, ngozi ikivutwa inarudi taratibu, kulegea, kuwa na hamu kubwa wa kunywa maji).

# MTU NI AFYA

Jamii bora huzingatia kanuni muhimu za afya. Asante kwa kusoma na kushiriki taarifa hizi na jirani, familia na marafiki zako.

Wizara ya Afya
Idara ya Kinga
Sehemu ya Epidemiolojia na Udhibiti wa Magonjwa

📞 Una tetesi au tukio la kiafya? Piga simu bure:

**199**

Huduma hii ni ya bure saa 24